

Waziri ahimiza vita ya ajira kwa watoto

Na Hellen Mlacky

WAZIRI wa Kazi na Ajira, Gaudentia Kabaka ameitaka jamii kushirikiana ili kukomesha utumikishwaji na ajira kwa watoto katika maeneo mbalimbali nchini ikiwemo katika mashamba, migodini, majumbani na uvuvi.

Waziri Kabaka aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam, wakati akizindua Mradi wa Kutokomeza Utu-

mikishwaji wa Watoto kwenye Mashamba ya Tumbaku (PROSPER) ambao utaendeshwa katika Wilaya za Urambo na Sikonge mkoani Tabora.

Alisema kuwa mpaka sasa serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wamewaondoa watoto zaidi ya 30,000 wenye umri chini ya miaka 14 kwenye ajira mbaya na kuwawezesha kupata elimu bora.

Alisema kuwa watoto wengi wamekuwa wakitumikishwa katika

mashamba ya mkonge, chai na tumbaku na wengine wakipewa majukumu ya nyumbani bila kuzingatia sheria zilizopo. Kabaka alisema kuwa mradi huo utasaidia kuwaondoa watoto hao katika ajira mbaya na kuwawezesha kwenda shule na hatimaye kuzisaidia familia husika kuondokana na umasikini.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa Mradi wa Prosper, Mary Kibogoya alisema kuwa mradi huo wa miaka mitano umelenga kusaidia

watoto 6,000 walio kati ya umri wa miaka 5-17 waishio katika mazingira magumu kuondokana na ajira hizo na hatimaye kupatiwa elimu.

Alisema mradi huo unaofadhiliwa na Mfuko wa Kupinga Ajira kwa Watoto katika Mashamba ya Tumbaku (ECLT) pia utaziwezesha familia zilizoiingizwa katika mpango huo kupata dola za Marekani 180 kwa mwaka kwa ajili ya ada ya mtoto na mtaji wa kuendesha biashara kwa ajili ya mama.